

Utenzi ufuatao ulitungwa awali na:
Bi Kidude wa Zanzibar na umeimbwa pia na
Jay Dee "Binti"

MUHOGO WA JANG'OMBE

1. Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Hadi tamati naapa, muhogo sitanunua
Haikuwa Maimuna, aliyekwenda ung'oa.
2. Kapata tetekuwanga, na ugonjwa wa surua
Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Kula dori kula dori, mshindo wa sufuria.
3. Gulili gulili, kofia inavuliwa
Ndie mimi ndie mimi, apatae ugoa
Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko.
4. Mtu akitaka kupa, hakuletei barua
Hukupa usingizini, pasi mwenyewe kujua
Kwenda mbio si kupata, bure unajisumbua
Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko.
5. Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Mkato wake matege, wakati anapokuja
Aliiweka dhamiri, ya kumvulia koja
Walahi nimeghairi, kiumbe ana mmoja.
6. Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Kamfunge kamfunge, beberu wa Athumani
Umfunge umfunge, pahala panapojaani.
7. Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Sina ngoa sina ngoa, kuhadaiwa sitaki
Ni mwerevu ni mwerevu, walahi sihadaiki.
8. Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Muhogo wa Jang'ombe, sijaulamba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko.